**LEARNING BY EAR 2012**

# “Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”

**EPISODE 6: ‘Ntapata wapi msaada? ’**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: MRS. RIMBA MEETS PRECIOUS AT THE SCHOOL**

- **Precious (f, 30)**
- **Mrs. Rimba (f, 45)**

**Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: JUDY AND HER TEAM AT KILINDI HIGH SCHOOL**

- **Judy (f, 40)**
- **Maneno (m, 45)**
- **Mixed voices (boys and girls 14-18)**
- **Pato (f, 16)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## UTANGULIZI:

Hujambo na karibu tena katika fursa hii ya Noa bongo, jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha sita katika hadithi inayoendelea ya **'Wasaliti walo karibu',** tukimulika maasi ya dhuluma za kingono barani Afrika. Kipindi kilichopita, Nuru alikwenda kituo cha polisi kupiga taarifa kuhusu masaibu yake ya ubakwaji lakini akakutana na kisiki cha ofisa kisicho hisia, mfano mzuri wa aina ya mtu asiyejali maslahi ya waathiriwa kama Nuru. Serefa, mamake Pato, alikwenda kumsabahi Pato shuleni mwake. Alikuwa na furaha pomoni kwa ajili ya matokeo ya Pato ijapo hakujuwa binti yake anapitia balaa gani. Kwengineko, Bi. Rimba, mwalimu wa Allan, alimtahini Allan ili aeleze kitu kinachomuudhi mno. Haya na leo riwaya hii itatufikisha wapi? Jawabu lipo katika kipindi hiki kiitwacho, **'Ntapata wapi msaada?'.** Tutaona mwanzo wa Allan akiwa shuleni, ambapo Bi. Rimba alimtaarifu mamake, Precious, aje kwa mazungumzo.

## SCENE ONE: BI. RIMBA AKUTANA NA PRECIOUS SHULENI

1. **SFX: SCHOOL BELL RINGS, OUTSIDE THE ROOM**

2. **PRECIOUS:** Naam, Bi. Rimba, mbona ukanialika nije haraka kukuona? Kumetokea nini huku shuleni?

3. **RIMBA:** Mama Allan… nakushangaa kwanini hujamkagua Allan akiwa ana miondoko ambayo sio kawaida yake.

4. **PRECIOUS:** Unamaanisha nini? Amefanya nini?

5. **RIMBA:** Hilo ni swali ambalo nadhani wewe, kama mama waweza kulijibu vizuri zaidi yangu... kwa ufupi, Allan amebadilika. Siye yule kijana nimjuae. Majuma machache tu alikuwa mchangamfu, mcheshi, na akifanya kazi zake vizuri shuleni; hata akifanya kazi zake za nyumbani na ni makini darasani. Siku hizi yupo yupo tu. Hajui kwaendelea nini, hapendi hata kucheza na wenzake, na ni nadra kumaliza kazi zake za shule.

6. **PRECIOUS:** Sasa wataka mimi nifanyeje? Mimi nafikiri nawalipa nyinyi walimu ili mniepushe na huu usumbufu. Au unataka mimi nimfanyie kazi zake za shule?

7. **RIMBA:** Mama Allan, kwanza ningekuomba ubadili mtazamo wako kuhusu suala hili. Ninachofanya ni kujaribu kumsaidia mtoto wako. Nahofia mgeuko wa ghafla wa tabia na miondoko ya kijana wako, hili laweza kuwa ishara ya shida au tatizo kubwa. Nimefanya utafiti wangu na nikagunduwa kinachomsumbuwa, sababu ninamjali sana mwanao.

8. **PRECIOUS:** **(shocked)** Kweli? Inaweza kuwa ni nini? Kijana wangu hakuna anachokosa.

9. **RIMBA:** Ijapokuwa sijui hususan ni nini, lakini uzoefu wangu katika kazi yangu unanionyesha Allan, amedhuriwa – kimwili au kihisia. Hicho ndicho chanzo cha matatizo yake.

**10. PRECIOUS:** Unasema nini eti? Bado sijakuelewa.

**11. RIMBA:** Mama Allan – upo uwezekano kuwa ameathiriwa... kimwili au labda hata ni…

**12. PRECIOUS:** **(defiant)** Ati nini?! Unawezaje kufikira hivyo! Ati unaniambia nini? Ati unanilaumu kuwa simchungi mtoto wangu? Na hilo jambo jengine ni nini? *Ati ameathiriwa*? La… la, hapana, sivyo, Bi. Rimba, nafikiri umevuka mpaka safari hii. Huna haki kufikiria hivyo kamwe…

**13. SFX: SHUFFLING OF PIECE OF PAPER**

**14. RIMBA:** **(interrupting)** Tazama majibu ya mtihani niliompa Allan afanye, ili nimdadisi kinachompa udhia. Tazama majibu aliyonipa.

**15. PRECIOUS:** **(reads out) '**Ni nini ninapendelea kufanya wakati wa ,mapumziko?'... **(Allan's answer) '**Hakuna.' 'Ni nani rafiki yangu mkubwa?' 'Sina!' 'Ni nani anayekuchukiza?' Naona, hili hakulijibu.

**16. RIMBA:** Ndiyo, hakujibu. Unaona alianza kuandika kitu alafu akafuta kabisa.

**17. PRECIOUS:** Sasa? Labda hakuna anayemchukia, anampenda kila mtu mtoto wangu .

**18. RIMBA:** Ni kweli kuwa ni kijana mzuri. Na ndiyo sababu kuu ya mimi kutaka kumsaidia. Watoto hufurahia kusema wanachopenda na wasichopenda, lakini majibu ya Allan aliyotoa, yalionyesha kuna shida. Ni kama anayehofia kitu au mtu...

**19. PRECIOUS:** **(shocked)** Siamini! Bi. Rimba, wewe ni mwalimu. Hebu nipe habari ulianza lini kazi ya upelelezi?

**20. RIMBA:** Mamake Allan, nimeamini hili ni jambo zito sana kwako, nisamehe kama nimekuudhi, lakini nasikitika kama hujajuwa kuwa dhulma za kingono hutekelezwa na watu wa karibu katika jamii zetu. Inasikitisha, siku za nyuma hata hapa shule kulitokea tukio la mwalimu kudhulumu watoto wa shule. Na wito ukatolewa wa kujizatiti kuzuia jambo hilo kabisa, na uamuzi ukawa mwalimu kupelekwa kwenye mafunzo yatakayowashauri na kuwasaidia waathiriwa hao. Na mwalimu ni mimi. Sasa, mama Allan, tafadhali fikiria: kuna mtu yeyote ambaye Allan anamuogopa kupita kiasi? Anaweza kuwa mtoto au hata mtu mzima?

**21. PRECIOUS:** **(angrily)** Hapana! Allan anaelewana sana na Uncle Joe. Hata hivi tusemavyo Uncle Joe amekuja kuishi na sisi na mtoto wangu ana heshima kuliko alivyokuwa awali.

**22. RIMBA:** Labda sitakusadikisha, na hata inaweza kuwa ni uongo, lakini hebu mchunguze huyu Uncle Joe, au hata labda ni kijana mwengine anaweza kuwa anamdhulumu kijana wako. Kwa sababu nikimchunguza alivyogeuka Allan, lazima kuna kitu kinamsumbuwa ambacho ni lazima sote tukivumbue.

**23. PRECIOUS:** **(totally shocked)** Ati! Una wazimu mwalimu wewe! Sitaki kusikia tena huu upuzi. la - ah, ah – ati unaniambia nini? Joe ni mtu mzuri, na mkarimu kuliko wote. Ni zaidi ya babake. Mwalimu Rimba labda akili yako imeruka, au labda… Huu wote ni wivu wako! Kwaheri, Bi. Rimba. Wasia mdogo, ningependa utazame kazi yako – wataka kazi, fundisha watoto lau hutaki! Acha!

**24. SFX: STEPS LEAVE, DOOR CLOSES ABRUPTLY**

**25. MSIMULIZI:** Kawaida ya binadamu kuwa mkaidi. Lakini sio suluhu kutosadiki. Mwalimu wa Allan ameng'amuwa kitu kuhusu Allan ambacho hata mamake hajajua, au amekataa kujijuza. Kwa jinsi anavyokataa maneno ya Bi. Rimba anavyomwambia, Precious anamweka kijana wake kwenye mnada. Lakini ni kawaida kwa wanadamu. Mapenzi ya jamii, wapenzi wao au hata majirani huwafanya wasikubali kuwa hawa huweza kuwaharibu watoto wao. Atajuta vipi Precious kwa ukaidi wake? Tutajua hivi karibuni. Lakini kwa sasa, tunakwenda shule nyengine: Pato anakosoma shuleni Kilindi, ambako Judy na shirika lake linalosimamia dhuluma za kingono, wamekuja kuwahamasisha wanafunzi kuhusu jambo hili la kulivalia njuga.

**SCENE TWO: JUDY NA PATO SHULENI KILINDI**

**26. SFX: NOISY MIXED HIGH SCHOOL ATMO**

**27. MANENO:** Haya hebu - kimya, kila mmoja! Utulivu! Nataka kila mmoja atulie tuli kama maji ya mtungi, hapa ndani.

**Silence**

**28. MANENO:** Kama mnavyojua mwalimu mkuu yuko mapumzikoni, kwa hivyo mimi ndiye mwenye kutoa amri kwa sasa. Sawa, leo tuna wageni watakao tuzungumzia mada muhimu sana. Nataka muwasikilize kwa makini watakayosema. Na mkumbuke ninawatazama ili nijue atakayekuwa hatilii maanani. Bi. Judy, sakafu ni yako.

**29. SFX: LOW NOISES AND MURMURS IN THE BACKGROUND**

**30. JUDY:** Asanteni, Bw. Maneno, na hadhira yote kwa ujumla. Kama mlivyosikia, jina langu ni Judy, na niko na wenzangu hapa kuzungumzia kuhusu ngono…

**31. SFX: WILD CHEERS AND UPROAR FROM MAINLY BOY STUDENTS**

**32. JUDY:** Haya. Sasa, maadamu sote tumemakinika, tuweni makini. Tuko hapa kuzungumzia dhulma za kingono. Kuna yeyote ajuae haswa dhulma hizi ni zipi?

**Total silence**

**33. JUDY:** Kwa ufupi, hili ni tendo lolote la ngono bila matakwa ya mwenye kufanyiwa, au pasipo hiyari. Yeyote anaweza kuathiriwa, lakini wengi ni wasichana wanaolengwa. Mtu anayefanya kosa hili daima huwa ni yule anayeaminiwa au jamaa: anaweza kuwa rafiki, mwanafunzi mwenzio darasani, jirani, ndugu, au hata mwalimu.

**34. SFX: SHOCKED, MIXED REACTIONS FROM STUDENTS**

**35. JUDY:** Ndio, najua hutaamini, lakini hutokea kila wakati, na ndiyo sababu ni muhimu kuzungumziwa. Naam, kuna njia nyingi za dhuluma za kingono – na sio lazima wakutane kimwili na muathiriwa. Kwa mfano, kumtusi mtu, maswala ya ngono, vitisho, au ukozimeni…

**36. SFX: BOY STUDENTS REPEATING THE WORD “KOZMENI?”**

**37. JUDY:** Wavulana… vijana, kama hamkujua haya kitambo, sasa mmejua, ukozimeni, ni hali ya kumchungulia mtu mwengine uchi wake. Kama nilivyotangulia kusema hapo awali, ni dhuluma iwapo mwenye kutendewa hakutaka kwa hiyari yake. Sidhani kama wasichana watatabasamu iwapo watagundua kuwa walikuwa wakichunguliwa uchi wao bila idhini.

**38. SFX: STRONG AFFIRMING ‘HAPANA’ REACTION FROM GIRLS**

**39. JUDY:** Hata hivyo – hatukuja kushtumu mtu hapa. Tumekuja kuwaelimisha mjue dhulma za kingono ni gani, na mtazizuia vipi. Utafiti umeonyesha kuwa, kwa wasichana wengi, tendo lao la kingono la kwanza ni ama limelazimishwa au amedhulumiwa. Lakini wengi huhofu kuripoti, kuhofia kejeli ya askari polisi, au kuwaeleza jamii na marafiki.

**40. (Mr. Maneno coughs several times and clears throat)**

**41. MANENO:** Samahani… sikupenda kukukatiza. Tafadhali endelea…

**42. JUDY:** Naam – asante sana. Waathiriwa wa dhulma za ngono pia huhofia kukejeliwa, kulaumiwa, au kukosa mtu wa kuwasaidia. Wengi huona haya au kudharauliwa. Wengine huamuwa kukaa kimya au hata kuogopa kwa sababu ya kutishiwa endapo watasema.

Sisi tunatoa msaada wa ushauri na matibabu. Njooni SUSV, Waathiriwa wote wanaombwa wasirudi nyuma, iwe ni kubakwa au dhulma nyengine yeyote. Tunakujali – tutakusikiliza, na tunaweza kukusaidia. Hata tunasaidia wanaohofu kupiga ripoti kituo cha polisi, kwa sababu ubaradhuli wa askari wetu tunaujua. Tungependa kuwauliza nyote msihofu, tusimame pamoja kukinga haya!

**43. SFX: SEVERAL PEOPLE CLAP THEIR HANDS**

**44. JUDY:** Hayo makofi machache yanatosha. Upo umuhimu wa kuwapa msaada waathiriwa. Hali yao inaweza kuwapa matatizo ya kudumu kiafya, mbali na majeraha ya mwili, unaweza kupata maradhi ya zinaa au mimba kwa wasichana na mama. Kihisia, hukosa maana ya kuishi ulimwenguni humu. Huhofia na kuogopa. Taswira hiyo mbaya hudumu, hukosa msimamo, na huishia kutumia vileo ili kujiburudisha akili zao. Wengine hupata maradhi mengine - ya kichwa, tumbo, kukosa hamu ya kula, kutolala, au maumivu ya mwili mzima. Yakizidi hapo mtu huamuwa hata kujitoa uhai wake.

**45. SFX: SHOCKED AND DISBELIEF REACTION FROM STUDENTS**

**46. JUDY:** Siyo hilo pekee: upo uhusiano mkubwa kati ya athari ya dhulma za ngono na matumizi ya mihadarati, matendo mengi ya kujitoa uhai, kukosa ari ya maisha na wasiwasi.

**47. SFX: SCHOOL BELL RINGS**

**48. JUDY:** Poleni kwa kuchukuwa muda wenu mwingi, lakini haya yanaweza kumtokea mtu yeyote, ndiposa nataka nyote muelewe – ili kumsaidia aliyedhulumiwa, au wewe mwenyewe. Nitaacha anwani yangu na Bw. Maneno, kama kuna mwenye swali, utawasiliana nasi. Shukran kwa kunisikiliza.

**49. SFX: HUGE ROUND OF APPLAUSE FROM STUDENTS**

**50. MSIMULIZI:** Judy na wenzake walitoka ukumbini na kulielekea gari lao lilioegeshwa nje ya lango la shule. Lakini kabla waondoke, Pato aliwafuata mbio huku machozi yakimtiririka.

**51. SFX: CAR STARTING AND ABOUT TO DRIVE OFF**

**52. PATO:** **(panting and crying uncontrollably)** Bi. Judy, nisubirini.... tafadhali msiende... ngojeni...

**HITIMISHO:**

Kilio cha kinyonge cha Pato kinatufikisha hatima ya kipindi cha sita cha dhulma za kingono. Kutatokea nini? Pato kweli atajieleza kwa Judy, ambaye hawajuani? Jiunge nasi kipindi kijacho. Unaweza kusikiliza kipindi hiki au kingine kilichotangulia kupitia wavuti wetu dw.de/lbe. Maoni yako tuma kupitia mtandao wetu wa Facebook. Mpaka wakati mwengine- Kwaheri.